# MUNGU WANGU

*Siku ya Mungu ya Matawi ABC*

**Mtunzi : MUHINDO NYENZE Charles**

**Maneno : Zaburi 21**




1.Wote wanaoniona wananicheka,
wanafumbua midomo , wanatikisa kichwa.
"Alimwamini Bwana , naye amwokoe;
amwopoe, kwani anampenda".

2.Kwa maana mbwa wengi wananizunguka,
kundi la waovu wananisonga,
wamenitoboa mikono na miguu,
naweza kuhesabu mifupa yangu yote.

3.Wanagawa nguo zangu kati yao,
wanaipigia kanzu yangu kura.
Nawe , ee Bwana , usisimame mbali:
Ewe tegemeo langu, fanya haraka kunisaidia.

4.Nitawahubiria ndugu zangu jina lako,
katikati ya mkutano nitakusifu.
"Enyi watumishi wa Bwana, msifuni,
Enyi wazao wote wa Yakobo, mtukuzeni:
mtumikieni, enyi waana wote wa Israeli."

*Fait à Buhimba , le 25 novembre 2018*